



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA MANISPAA KIGAMBONI**



Kumb. Na. EB.60/315/02/13

Tarehe: 20/01/2025

**TANGAZO KWA UMMA KUHUSU MIKOPO INAYOTOLEWA KWA  
VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU**

(LIMETOLEWA KWA KUZINGATIA KANUNI YA 7 (1))

**MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI ANATANGAZA UWEPO WA FEDHA KWA AJILI YA KUVIKOPESHA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU, AMBAPO JUMLA YA TSH. 1,281,021,850.85 ZIMETENGWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2024/2025. HIVYO VIKUNDI VYENYE SIFA VINAKARIBISHWA KULETA MAOMBI KATIKA OFISI ZA SERIKALI ZA MITAA/KATA ZILIZOPO KATIKA MAENEO YENU.**

**VIKUNDI VINAVYOTAKIWA KUOMBA MKOPO VINAPASWA KUWA NA SIFA ZIFUATAZO;-**

**(I) KIKUNDI CHA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU KILICHOTAMBULIWA NA KUPEWA CHETI CHA UTAMBUZI NA HALMASHAURI.**

**(II) KIKUNDI KIWE KINAJISHUGHULISHA NA SHUGHULI ZA UJASIRIAMALI MDOGO AU WA KATI AU KIKUNDI KINACHOTARAJIA KUANZISHA SHUGHULI ZA UJASIRIAMALI.**

**(III) KIKUNDI CHA WANAWAKE NA VIJANA KIWE NA IDADI YA WANAKIKUNDI KUANZIA WATANO (5) NA KUENDELEA NA KIKUNDI KIWE CHA WATU WENYE ULEMAVU KIWE NA WANAKIKUNDI WASIOPUNGUA WAWILI (2). PIA KWA KUZINGATIA KANUNI YA 6 (1) MTU MWENYE ULEMAVU ANAWEZA KUWA NA SIFA YA KUPATA MKOPO KAMA KIKUNDI CHA WATU WENYE ULEMAVU ENDAPO TIMU YA MENEJIMENTI YA HALMASHAURI ITAJIRIDHISHA KUWA AMEKOSA MTU MWINGINE MWENYE ULEMAVU WA KUUNGANA NAYE KATIKA ENEO LAKE. AIDHA SIFA ZINGINE ZITAFANANA SIFA ZA VIKUNDI VINGINE.**

(IV) KIKUNDI KIWE NA AKAUNTI YA BENKI ILIYOFUNGULIWA KWA JINA LA KIKUNDI KWA AJILI YA MATUMIZI YA SHUGHULI ZA KIUAJASIRIAMALI; NA

(V) WANAKIKUNDI LAZIMA WAVE RAIA WA TANZANIA WASIO NA AJIRA RASMI WENYE AKILI TIMAMU NA WENYE UMRI KUENZIA MIAKA 18 NA KUENDELEA . AIDHA KIKUNDI CHA VIJANA KITAPASWA KUWA NA WANAKIKUNDI WENYE UMRI KUENZIA MIAKA 18 HADI 45.

MAOMBI YOTE YATUMWE KUPITA MFUMO WA KIELEKTRONIKI (TEMBELEA TOVUTI: MIKOPOHALMASHAURI.TAMISEMI.GO.TZ) ILI KUTAMBULIWA NA KUOMBA MKOPO WASILIANA NA AFISA MAENDELEO YA JAMAI WA KATA HUSIKA AU MTENDAJI WA KATA HUSIKA.

KIKUNDI KINACHOMBA MKOPO KINAPASWA KUWA NA VIAMBATISHO VIFUATAVYO; BARUA YA KIKUNDI YA KUOMBA MKOPO ILIYOPITISHWA NA AFISA MTENDAJI WA KIJIKI/KATA, MUHTASARI WA KIKUNDI WA KUOMBA MKOPO, ANDIKO RAHISI LA MRADI UNAOOMBWA MKOPO KWA KUZINGATIA FOMU ILIYO NDANI YA MFUMO NA TAARIFA YA AKAUNTI YA BENKI.

MWISHO WA KUWASILISHA MAOMBI NI TAREHE 20 MWEZI 2 MWAKA 2025

TANGAZO HILI LIMETOLEWA LEO TAREHE 20/01/2025

*Erasto*

ERASTO N. KIWALE  
MKURUGENZI WA MANISPA  
HALMASHAURI YA MANISPA

